(INSHA NA UTANGULIZI WA FASIHI)

Jina ______________________ Nambari ya usajili __________

Shule ______________________ Tarehe __________

Maagizo: JIBU MASWALI YOTE

MUDA: SAA 1 DAK 40

## ZOEZI 1: INSHA (Alama 20)

1. **Endeleza insha ifuatayo iwe ya kuvutia na ya kusisimua.**

Dawa za kulevya zimepigwa marufuku katika taifa letu la Kenya ........................................

**SEHEMU YA B: (Alama 30)**

**ZOEZI II: FASIHI SIMULIZI (Alama 10)**

2. **Soma hadithi hii kisha ujibu maswali yafuatayo**

Sungura alijidai mwerevu. Aliwaona wanyama wenzake kuwa wajinga sana. Hakujua kuwa pwagu anaweza kupata pwaguzi. Sungura alianzisha biashara ya kuwekea wanyama pesa benkini. Kobe alikuja kuweka pesa zake. Baada ya muda, kobe aliendа kutoa hela kidogo. Sungura alimkataza kobe kutoa pesa kidogo.

Alisema, "Huwezi kutoa hela chache hivyo. Hatutaki maskini. Hii ni benki ya matajiri," Sungura alisema kwa ukali.

"Sawa. Wacha ukali. Upole utakufaa. Sipendi ubishi. Nitatoa pesa zangu zote. Naomba unihesabie," Kobe alisema kwa unyenyekevu. Sungura aliangalia akaunti ya kobe. Alishangaa kuona kuwa kobe alikuwa na mabilioni ya pesa. Alianza kumuomba Kobe msamaha kwa ujeuri wake.

"Usinione hivi. Najiamini na kujithamini ndugu yangu. Uvumilivu wangu umekupa funzo," Kobe alimwambia sungura kwa upole kisha akaondoka.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**(a).** Taja wahusika wawili katika hadithi hii (al 2)

________________________________________

**(b).** Eleza maana ya methali **"Pwagu hupata pwaguzi"** kama ilivyotumika katika hadithi hii (al 2)

________________________________________

________________________________________

**(c).** Fafanua shughuli aliyohusika nayo Sungura (al 2)

________________________________________

**(d).** Taja sifa **mbili** za Kobe kutokana na hadithi uliyosoma. (al 2)

(i). ________________________________________

(ii). ________________________________________

**(e).** Ni funzo lipi umejifunza kutokana na taarifa hii? (al 2)

________________________________________

**3. ZOEZI YA III: Novela (Alama 10)**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali**

Mungu Muumba alifanya kazi yake ya uumbaji na akaikamilisha sawa sawa. Alimweka binadamu mwenye akili kuwa mtunzi na kiongozi wa viumbe wengine. Binadamu huyu amegeuka hayawani kwa kutumia mazingira yake visivyo.

Ukweli wa mambo ni kwamba, katika majiji na vijiji vingi humu nchini huwa na majalala na mabiwi ya takataka ambayo yamesambaa kote kote. Wananchi wengi wakubwa kwa wadogo, vijana kwa wazee, wanawake kwa wanaume hutupa taka shaghalabaghala. Si vinyesi vya watu, si maganda na mabaki ya vyakula, yote yametapakaa vichakani, vijiani, sharobani na kandokando za baraste mijini na vijijini. Ukitembea maeneo kama haya utakereketwa moyoni na kujiuliza; Je, wale wanaofanya haya wana fikira razini? Jiamulie mwenyewe. Jambo kama hili hushusha hadhi ya insi.

Pana mahali mwafaka ambapo taka hutupwa. Mapipa yamewekwa katika sehemu mbalimbali mijini ambayo hukudhihirishia mahali pa kutupa taka.

Ni wajibu wa kila mmoja kuyatumia mapipa hayo. Ukila tunda au ukinywa maziwa, hakikisha kuwa mabaki yametupwa humo. Vile vile, kuna vyoo ambavyo vinatakiwa kutumiwa vilivyo, kuwe ni mashambani au mijini.

Ni jukumu letu binadamu kuhakikisha kuwa tunaishi katika mazingira safi ili kuepukana na kuambukizwa magonjwa mbalimbali kama vile waba na homa ya matumbo. Kuyahifadhi mazingira yetu vizuri ni sharti tushirikiane katika kuyanadhifisha. Wahenga hawakukosea walipoamba kuwa "Jifya moja haliinjiki chungu"

**(a).** Binadamu amegeuka hayawani kwa (al 2)

________________________________________

**(b).** Wanaochafua mazingira ovyo ovyo ni (al 2)

________________________________________

**(c).** Mahali paikutupa taka panaitwaje (al 2)

________________________________________



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

(c). Tumeshauriwa kuishi katika mazingira safi ili (al 1)

_______________

(d). Andika methali nyingine iliyo na maana sawa na **"Jifya moja haliinjiki chungu"** (al 1)

_______________

(e). Neno jingine lenye maana sawa na 'waba' ni (al 1)

_______________

(f). Eleza funzo ulilopata kutokana na taarifa hii. (al 1)

_______________

**ZOEZI IV: USHAIRI (Alama 10)**

4. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Saba nakupa kwaheri, nane sasa navukia,
Ulotupa ni bahari, upeo kuashiria,
Taimba zako habari, historia kumbukia,
La saba sasa kwaheri, twaelekea la nane

Jahari litupokeza, na mema maandalzi,
Tuendapo tasambaza, wengi wapate ujuzi,
Elimu taangaza, kuhifadhi kumbukizi,
La saba sasa kwaheri, twaelekea la nane.

Ulotujuza ni mengi, baadhi yao tataja,
Kwanza majina ya rangi, za kiswahili lahaja,
Za kulevya kama bangi, kamwe hatuwi wateja,
La saba sasa kwaheri, twaelekea la nane.

(a). Shairi hili ni la aina gani? (al 1)

_______________

(b). Eleza ujumbe wa mwandishi katika ubeti wa kwanza (al 1)

_______________

(c). Taja mambo **mawili** aliyojifunza mshairi (al 2)

(i). _______________

(ii). _______________

(c). Andika kibwagizo cha shairi hili. (al 1)

_______________

(d). Shairi hili lina ubeti ngapi? (al 2)

_______________

(e). Pendekeza kichwa kinachofaa katika shairi hili. (al 2)

_______________

(f). Mshororo wa kwanza katika ubeti wa kwanza una mizani ngapi? (al 1)

_______________



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com